

**Ufahamu wa usalama na mahitaji ya afya katika mahali pa kazi**

**Taarifa Rasmi**

***Kielekezi kwa maana ya wafanyakazi wahamiaji***

Katika Magharibi Australia, sheria huhitaji kuwepo kwa kiwango cha juu cha usalama kutolewa katika mahali pako pa kazi, na kuwa haudhuriki au kuumia kwa ajili ya kazi. Kufanya mahali pa kazi kuwa salama hutegemea mwajiri na mfanyakazi kufanya kazi kwa kuungana pamoja.

Waajiri wana jukumu kutoa kama iwezekanavyo mahali salama pa kazi. Hii huitwa ‘wajibu wa utunzaji’. Wewe kama mfanyakazi pia una wajibu wa utunzaji wa kufanya kazi kwa usalama pamoja na kutoathiri usalama na afya yaw engine.

Sheria katika Magharibi Australia pia huhitaji mwajiri kufikiria mahitaji ya kibinasi ya wafanyakazi kwa kuandaa mahali salama pa kazi. Kwa mfano, wanahitajika kufikiria jinsi ya kuwajulisha maelezo kuhusu usalama kwa wale walio na upungufu wa maarifa ya kiingereza, au wale walio na mahitaji ya kimaalum.

**Kushiriki katika maswala ya usalama katika mahali pa kazi**

Kama mfanyakazi, kunazo njia tofauti unazoweza kushiriki katika kuhakikisha usalama na afya katika mahali pako pa kazi. Unaweza kufanya hivi kwa:

- Kuongea moja kwa moja na mwajiri, msimamizi na wafanyi kazi wenzako kuhusu mashaka unayoweza kuwa nayo;
- Kumjulisha msimamizi au mwajiri kuhusu madhara au maumivu, madhara au maumivu yanayowezekana;
- Kushiriki katika mafunzo ya utaratibu usio fahamu;
- Kuuliza maswali kuhusu maswala yeyote usioelewa;
- Panapo hitajika, kuomba maelezo na mafunzo kutolewa kwa umbo linalohitajika ili kutimiza mahitaji yako, kwa mfano kupitia mtafsiri au mkalimani; pamoja na
- Palipo na wawakilishi wa usalama na afya au kamati ya usalama na afya, jadiliana suala nao.

Kunayo maelezo kwenye tovuti ya WorkSafe kuhusu jinsi ya kufanya hivi. WorkSafe ni ofisi ya wakala ya serikali iliyo na uwezo wa kushurutisha utiifu wa sheria za usalama na afya kazini pamoja na kuchunguza mashaka kuhusu mahali pa kazi pasipo na usalama. WorkSafe pia inayo kituo cha maelezo, ambacho waweza kupiga simu ukiwa na shaka au ukihitaji maelezo. Unaweza kuuliza kuwa hoja zako zibakie siri na kuwa maelezo yako yasipewe mtu yeyote.

WorkSafe

Level 5, 1260 Hay Street, WEST PERTH WA 6005

Simu: 1300 307 877

Nukushi: (08) 9321 8973

Barua pepe: safety@commerce.wa.gov.au

Tovuti: [www.worksafe.wa.gov.au](http://www.worksafe.wa.gov.au)

<b>Ratiba ya haki na majukumu</b>	
	<p>Mwajiri wako ana jukumu ya kuhakikisha kuwa:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>– Umefunzwa kufanya kazi kwa usalama;</li> <li>– Unajua kuhusu hatari na mashaka yanayohusika na kazi yako;</li> <li>– Unajua jinsi ya kutumia vifaa, mashine na vitu vinavyohitajika kufanya kazi kwa usalama na bila mashaka ya afya yako;</li> <li>– Unajua jinsi ya kutumia na kutunza usalama na vifaa vya kujikinga kibinafsi;</li> <li>– Unajua jinsi ya kutatua malalamiko yoyote au mashaka kuhusu usalama;</li> <li>– Unajua jambo la kufanya kama kukitokea jambo la dharura;</li> <li>– Unajua jambo la kufanya kama ukiumia;</li> <li>– Unajua haki zako za ridhaa kama ukiumia;</li> <li>– Unajua unayo haki ya kuwacha kazi kama ukifikiri uko hatarini pamoja na</li> <li>– Unajua jinsi ya kuwasiliana na WorkSafe ili kukusaidia na mashaka ya usalama.</li> </ul>
	<p>Ili kuhimiza jukumu zako za usalama na afya katika kazini, unayo jukumu ya:</p> <ul style="list-style-type: none"> <li>– Kufuata maagizo yaliyotolewa kuhakikisha usalama na afya kazini;</li> <li>– Hakikisha matendo yako kazini hayasababishi hayaumizi watu wengine;</li> <li>– Ripoti hatari, maumivu au afya iliyodhoofika kwa msimazi pamajo na/au mwajiri;</li> <li>– Tunza usalama pamoja na vifaa vya kuchunga usalama kwa njia uliyofunzwa na uripoti mashaka yoyote yanayohusu vifaa hivi;</li> <li>– Fuata utaratibu wa dharura kama inavyohitajika; pamoja na</li> <li>– Uliza kama huelewi maelezo uliyopewa.</li> </ul>

### ***Nyenzo zaidi***

#### *Unions WA*

Unions WA ni muungano wa kundi la serikali linalowakilisha zaidi ya miungano arubaini zinazoshirikiana, pamoja na wanachama. Miungano ayweza kupeana ushauri kwa haki za wafanyi kazi.

Level 4, 445 Hay Street, PERTH WA 6000

Simu: (08) 9328 7877

Nukushi: (08) 9328 8132

Barua pepe: [unionsyes@unionswa.com.au](mailto:unionsyes@unionswa.com.au)

Tovuti: [www.unionswa.com.au](http://www.unionswa.com.au)

#### *WorkCover Magharibi Australia*

WorkCover WA ni wakala ya serikali ilinayoshughulikia ridhaa ya wafanyikazi na utawala wa maumivu.

2 Bedbrook Place, SHENTON PARK WA 6008

Simu: (08) 9388 5555

Nukushi: (08) 9388 5550

Tovuti: [www.workcover.wa.gov.au](http://www.workcover.wa.gov.au)